

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

*Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Baruapepe : press@ikulu.go.tz  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)*



*OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.*

*Dodoma  
13 Desemba, 2023*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Bodi kama ifuatavyo:

- i) Amemteua Jaji Mshibe Ali Bakari kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (Tanzania Meteorological Authority - TMA) na amemteua Dkt. Emmanuel Jonathan Mpeta kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo.
- ii) Amemteua Balozi Adadi Mohamed Rajab kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa binafsi na amemteua Bi. Fatma Mohamed Ali kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo.
- iii) Amemteua Bw. Theobald Maingu Sabi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Mkonge, Tanzania.

Uteuzi huu umeanza tarehe 10 Desemba, 2023.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Zuhura Yunus".

Zuhura Yunus  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

